**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI WA MBULU**

**SHULE YA SEKONDARI KAINAM**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAINAM

**12, Juni, 2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu- 0621-5564-07**

**Mkuu wa Shule EMANUEL N. MADME**

**Makamu Mkuu wa Shule AGATON DIYAMI**

**Matron/Patron LUCY B. BOA**

**Shule ya Sekondari KAINAM**

**S.L.P 158**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAINAM HALMASHAURI YA MBULU MJI MKOA WA MANYARA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari KAINAM ipo umbali wa Kilometa 12 kusini mashariki mwa Mji wa Mbulu Usafiri wa haysi na bodaboda kutoka mjini Mbulu hadi Kainam unapatikana katika stendi ya Kainam Nauli ni Shilingi haysi 2000/= na kwa pikipiki na Shilingi 4000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

#### (a) Wasichana

- Sketi mbili (2) rinda box, rangi ya dark blue (grade one). Urefu wa sketi ni nchi nane (8) kutoka magotini kwenda chini, "belti yenye inchi mbili (2) na pindo la chini liwe la wastani,
- mashati meupe mawili tetron mikono mirefu,
- Tai 2 rangi ya dark blue yenye mfanano wa rangi ya sketi
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi,
- Sweta rangi sawa na sketi
- Soksi ndefu nyeupe (stoking) jozi mbili au zaidi

#### (b) Wavulana

- Suruali mbili (2) za rangi ya dark blue zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) la upana wa nchi 18 (suruali zilizobana au modo hazitaruhusiwa) na mkanda mweusi wa ngozi,
- Mashati mawili meupe mawili (02) au zaidi ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja.
- Mashati meupe ya tomato yanashauriwa Zaidi,
- Viatu vya rangi nyeusi vya kufunga na kamba na visiwe na visigino virefu pamoja
- soksi ndefu nyeupe jozi mbili au Zaidi**,**
- Nguo za michezo ni Tracksuit ya rangi ya **damu ya mzee/maruni** (yenye mistari myeupe ubavuni) isiyo na maandishi, raba na soksi za blue.
- Sweta la dark blue lenye V - shingoni
- Traki suit rangi ya blue masai (hizi ni sare za shule ambayo ina siku ya kuvaliwa katika wiki)
- Traki ya kushindia na kuvaa muda wa maandalizi ya usiku (night preparation) rangi nyekundu yenye kofia
- T-shirt za shule (zinapatikana jirani na Shule kwaTsh 15,000/= siku ya kuripoti )

- Nguo za kushindia ni fulana (Tshirt) mbili (02) au zaidi zenye kola na mikono mifupi rangi ya blue na sizizo na maandishi.
- Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
- Viatu vya wazi (sandals) kwa ajili ya kushindia. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa ndala wala yeboyebo. Yeboyebo zitatumika bafuni na maliwato tu.

i. Mashati **meupe mawili tetron mikono mirefu** (*taja idadi na aina*);

ii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe visivyo na marembo yoyote ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*ambatisha mshono*);

**Sare ya Michezo ni**

Kwa wasichana T- Shirt rangi ya njano, Traki suti rangi ya blue bahari, Traki ya kushindia rangi nyekundu yenye kofia, Raba jozi moja za michezo, Soksi za michezo jozi mbili na Bukta rangi nyekundu na **T- shirt rangi ya njano, Traki suti rangi ya maron au damu ya mzee, Raba jozi moja za michezo, Soksi za michezo jozi mbili au Zaidi, Bukta rangi nyekundu** kwa wavulana

iii. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

iv. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vi. Sweta dark blue

vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*)

**WASICHANA**

- Sketi mbili rangi ya ugoro au chocolate
- Mabuti ya mvua rangi nyeusi au kijani jozi moja (1)
- Mwavuli moja kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika
- Raba nyeupe au nyeusi (mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au yebo nje ya bweni au darasani) ndala au yeboyebo ni kwa ajili ya matumizi ya kuoga tu

- T-shirt ya blue moja au zaidi

**WAVULANA**

- Suruali rangi ya ugoro au chocolate
- Mabuti ya mvua rangi nyeusi au kijani jozi moja (1)
- Mwavuli moja kwa ajili ya kujikinga na mvua kipindi cha masika
- Raba nyeupe au nyeusi (mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au yebo yebo nje ya bweni au darasani) ndala au yeboyebo ni kwa ajili ya matumizi ya kuoga tu
- T-shirt ya kijivu moja au zaidi

viii. Tai ya dark blue

ix. Tisheti (T-shirt) wasichana blue na wavulana kijivu

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 8

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*kila mwanafunzi aje na vitabu vya masomo anayosoma)*

iv. Scientific Calculator kwa wanaosoma jeografia

v. Godoro inchi $2\frac{1}{2}$ kwa wanafunzi wa Bweni

vi. Mashuka blue bahari Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro blue bahari1, chandarua nyeupe 1

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Mathematical set 1 kwa wanaosoma jeografia

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. HGK: Aje na mopa, jembe na mpini pamoja na panga.
HKL: Aje na hardbroom, jembe na mpini pamoja na panga.

**N.B** vifaa vifuatavyo vinapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya sokoni ”mashuka, madaftari, kalamu, sahani, vikombe, vijiko, mathematical set, mswaki na dawa ya meno”

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

# 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## SHULE YA SEKONDARI KAINAM

ORODHA YA VITABU

Orodha ya vitabu vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa yaani HGK (History, Geography na Kiswahili) au HKL (History,
Kiswahili na English Language). General studies ni kwa wote.

### A. HISTORY

1. TIE (2016) History for Secondary Schools: Form Five - Tanzania Institute of Education.
2. TIE (2016) History for Secondary Schools Form Six, Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education
3. Tumaini, S.C.K (2010) Contemporary Historical Events: Advanced Level History one, Dar es Salaam:
Shgibitali & Sons publishers
4. Yassin S. (..) Essentials in Advanced Levels History Paper 2, Dar es Salaam

### B. ENGLISH LANGUAGE

1. Asheri, N. (2014) Advanced Level English: A Practical Approach,3rd Ed., Dar es Salaam: Good Books

Publishers

2. John, J. (2012) Advanced English Language: Form 5 & 6, Dar es Salaam: Oxford University Press.

3. TIE (2016) English Language for Secondary Schools: Literature and Stylistics Form Five and Six, Dar es
Salaam: Tanzania institute of Education

## POETRY

(a) Selected Poems. - Tanzania Institute of Education

(b) The wonderful Surgeon and Other Poems. – Charles Mloka - Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

## NOVELS AND SHORT STORIES (walau vitabu viwili)

(a) The Beautyful Ones Are Not Yet Born - Ayi Kwei Armah

(b) A Man of the People - Chinua Achebe

(c) Divine Providence - Severin N. Ndunguru

(d) His Excellence Head of State - Danny Safo

(e) Encounters from Africa – Macmillan Education Limited

## PLAYS (walau vitabu viwili)

(a) Betrayal in the City - Francis Imbunga

(b) I Will Marry When I Want - Ngugi wa Thiong'o and Ngugi wa Mirii

(c) Lwanda Magere - Okoiti Omtatah

(d) An Enemy of the People - Henrik Ibsen

(e) Black Mamba - John Ruganda

## C. GEOGRAPHY

1. Geography for Secondary Schools: Form Five. - Tanzania Institute of Education (2016)

2. Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying. – Zisti Kamili

3. Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges. – Ahmed Lubwama

4. A Comprehensive Approach to Physical Geography – D.T. Msabila

## D. KISWAHILI

(i) KISWAHILI 1

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010)

2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)

3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI

(ii) FASIHI

1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford university Press

2. Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangwine na Masebo

### TAMTHILIA (walau vitabu viwili)

1) Kivuli Kinaish – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press

2) Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press

3) Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)

4) Morani –Emanuel Mbogo (1993)

### RIWAYA (walau vitabu viwili)

1) Vuta ni Kuvute, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)

2) Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota

3) Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan

4) Usiku Utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

## USHAIRI (walau vitabu viwili)

1) Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed.) – Haji Gora Haji (1995) - TUKI

2) Chungu Tamu – Theobald Mvungi

3) Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers

4) Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

## E. GENERAL STIUDIES

1. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General
Studies Notes form 5 & 6.
2. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level
Secondary Schools,

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………....……………..Age…….…Sex…………year…..

1. Blood count (Red and White) ……………………………………...
2. Urinalysis Test ……………………………………………………….
3. Syphilis test…………………………………………………………
4. T.B……………………………………………………………………
5. Eye Test ……………………………………………………………
6. Ears…………………………………………………………………
7. Spleen………………………………………………………………
8. Abdomen ………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

……………………………. …………………………………

Name and Designation Signature and Official stamp

……………………………. ……………………………

STATION DATE

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.

Thank you in advance

…………………………………

EMANUEL N. MADME

HEAD MASTER

KAINAM SECONDARY SCHOOL

# Fomu Na. 2
# AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ________________________________Wa kidato cha Tano chaguo_______________(tahasusi) mwaka wa masomo 2023/2024. Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Kainam.
Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla

katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni, ili niweze kupata elimu na

kuendeleza jamii na Taifa langu.

Ninaahidi na kukiri kuwa sintashiriki kwenye mgomo kwa namna yoyote ile.

Jina:______________________________ Saini________________

Tarehe: ____________________

# Fomu Na. 1

# AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi________________________wa S.L.P______Mji___________Simu ______________ Ambaye kazi yangu ni _______________natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ____________________. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Kainam kuanzia tarehe ___________________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina:____________________________ saini__________________

Tarehe:______________ Uhusiano na mwanafunzi:____________

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule EMANUEL N. MADME**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0621-556407**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0622-457556**
- **Mwandamizi Taaluma 0623-429941**
- **Mwandamizi Malezi 0623-842740**

Mwisho Kwa niaba ya jumuiya ya Kainam sekondari napenda kukukaribisha Sana hapa shuleni na kukutakia safari njema na mafanikio mema katika masomo yako ya kidato cha tano na sita.

**“Almight the lord grants and blesses you abundantly”**

……………………..

EMANUEL N. MADME
MKUU WA SHULE
0621-556407